**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**

Shule ya Sekondari Sumve,
S. L. P 44,
Mantare – Mwanza.

27/04/2022

**Namba za simu**
Mkuu wa shule 0769969156
Makamu wa Mkuu wa shule 0767419328
Matron (2) 0764765370
Patron 0753 020 670

Kumb. Na: SHS/F.5/Vol.1/2022
Mzazi wa ……………………………………………………
S.L.P…………………………………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SUMVE HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA MKOA WA MWANZA MWAKA 2022.**

i. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **Tano** katika shule hii mwaka 2022 katika tahasusi ya …………. **"HONGERA SANA".** Mwanao anatakiwa kuripoti hapa shuleni **tarehe ……/…./2022 na masomo yataanza rasmi tarehe …../…./2022** bila kuchelewa. Tafadhali zingatia maelekezo yote kwa umakini ili mwanao asije akapoteza nafasi yake. Pindi mwanao atakapokuja alete kivuli cha cheti cha matokeo "Result Slip" na kivuli cha cheti chake cha kuzaliwa. Kama hana cheti cha kuzaliwa, ajaziwe fomu ya uraia (ithibitishwe na **WEO** au **VEO** wa eneo atokalo). Pia ajaziwe fomu ya vipimo vya afya na fomu ya maelezo juu ya mwanafunzi. Fomu zote hizi zimeambatanishwa pamoja na barua hii. Hakikisha zimejazwa kikamilifu kwa mujibu wa maelekezo, kisha mwanafunzi aje nazo siku ya kuripoti.

**MAHALI SHULE ILIPO.**

Shule ya sekondari SUMVE (**Sumve High School**) ipo katika wilaya ya Kwimba, Mkoa wa Mwanza kilometa zipatazo 45 kusini – mashariki mwa jiji la Mwanza. Endapo utatumia usafiri wa basi, kwa watakaotokea njia ya shinyanga kuelekea Mwanza, teremkia kituo kikuu cha basi cha NYEGEZI, au popote pale utakapoteremshiwa mjini utakuta daladala ziendazo IGOMA au KISESA. Panda na teremkia kituo cha mwisho kabisa (KISESA). Ukifika KISESA utapata usafiri wa SUMVE, utateremshiwa Stand ya Sumve na shule iko hatua chache kutoka stand ilipo.
Kwa watakaosafiri kwa meli au vivuko vya ziwani, mara tu watakapowasili bandarini, wataoneshwa hizo daladala za kutoka mjini kwenda KISESA. Ukitumia njia kutokea Musoma kuelekea Mwanza, uteremshiwe KISESA moja kwa moja.

Iwapo utatumia usafiri wa Ndege, ukifika Airport ya Mwanza, panda teksi hadi KISESA. Pia unaweza kutumia usafiri wa daladala ziendazo KISESA. Kwa kawaida, usafiri wa kuelekea Sumve kutoka KISESA upo wakati wote, na usafiri wa mwisho ni saa 12:00 jioni

****************** KARIBUNI SANA **********************

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

2**.1 Sare ya shule**

**a) sare za darasani**

- Sketi 2 za marinda manane (mawili kila upande kulia na kushoto) - kitambaa cha suti rangi ya dark blue, ziwe ndefu mpaka kwenye fundo za miguu, zinapatikana shuleni au anaweza kushonea nyumbani kama zinavyoonekana kwenye kiambatisho (picha). Bei ya sketi moja ni 20,000/=
- Shati 2 nyeupe zenye mikono mirefu (Tomato) zinapatikana duka la shule @ Tsh 12,000/= Hijabu 2 zilizoruhusiwa kisheria. (kwa waislam) zinapatikana shuleni @ sh 18,000/= au anaweza kuja nazo.
- Aje na shimizi au sidiria (rangi nyeupe au nyeusi tu).
- Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi visivyokuwa na mapambo ya aina yoyote.
- Soksi jozi mbili nyeupe. (zinapatikana duka la shule kwa kila jozi Tsh 1,000/=.
- Sweta 1 la bluu (Pia linapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/=) au anaweza kuja nalo.
- Tai 1(Zinapatikana shuleni kwa Tsh 5,000/=)

**b) Sare za kushindia**

- Sketi mbili za marinda mengi za kushindia kitambaa cheusi cha suti, ziwe ndefu mpaka kwenye fundo za miguu zinapatikana shuleni. Bei ya sketi moja ni 20,000/= au anaweza kuja nazo.
- T shirt 2 za kola za kushindia (zinapatikana shuleni @ Tsh 12,000/=)
- Suruali nyeusi ya kitambaa (sio jeans) kwa ajili ya kusomea wakati wa 'prep' usiku, na sio vinginevyo.

c) **Sare za michezo**

- Sare za michezo raba rangi nyeupe, soksi za bluu na track suit (soksi sh.1,500 na track suit Tsh. 25,000/= zinapatikana shuleni).
- T shirt ya bluu 1 zinapatikana shuleni kwa bei ya sh 7,000/=

**NB: Michango ya sare za shule italipwa shuleni moja kwa moja na siyo kwenye akaunti ya shule.**

**2. 2 Ada na michango ya shule**

- Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= kwa wanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa maramoja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule katika Benki ya **NMB A/C 31501100461 (jina la A/C SUMVE HIGH SCHOOL)** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

**Michango ya shule**

**a) Michango ya shule inayolipwa kwenye Akaunti ya shule**

i. Sh. 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
ii. Sh. 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
iii. Sh. 20,000/= kwa ajili ya taaluma kwa mwaka.
iv. Sh. 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi, mpiga chapa na vibarua wengine.
v. Sh. 2,000/= nembo ya shule.

vi. Sh. 20,000/= mazoezi mbalimbali ya kitaaluma.
vii. Sh. 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza shuleni na na siyo kwa ajili ya matibabu iwapo mwanao atalazwa hospitali (kama mwanao ana magonjwa ya kudumu au ya mara kwa mara,

tunakushauri umkatie BIMA ya afya ya mwaka ya TAIFA (NHIF) ambayo itamuwezesha kutibiwa sehemu yoyote ile ndani ya nchi na huduma hiyo inapatikana ofisi za BIMA YA AFYA KWA WILAYA ZOTE)
viii. Fedha ya tahadhari sh.5,000/= (haitarejeshwa).

**NB: Pesa ya michango ya shule ilipwe kwenye tawi lolote la NMB A/C N0 tajwa hapo juu. Mzazi/mwanafunzi alete pay- in – slip ya Benki halisi na sio kivuli cha pay in – slip.**

**b) Michango ya shule isiyolipwa kwenye akaunti ya shule**

i. Ujenzi wa uzio wa shule Tsh 50,000/= rejea kikao cha wazazi cha tarehe 11/09/2020.
ii. File 2,000/=
iii. Mchango kwa ajili ya utengenezaji wa vitanda Tsh 25,000/= kwa kila mwanafunzi. rejea kikao cha wazazi cha tarehe 11/09/2020.
iv. Mchango wa sh 5,000/= kwa mwezi kwa ajili ya masomo ya ziada (remedial programme) hii ni kwa mujibu wa makubaliano ya kikao cha wazazi. rejea kikao cha wazazi cha tarehe 11/09/2020.
v. Ream ya karatasi 1 (kwa muhula) aina ya double A zinapatikana kwenye duka la shule kwa bei ya sh 12,000/= au aje nayo.
vi. Scientific calculator kwa michepuo ya EGM na HGE (mzazi anaweza kununua kwenye duka la shule 50,000/=)
vii. Aje na sh. 20,000/= kwa ajili ya kulipia godoro, kwa mwaka.
viii. Mashuka 2 ya pinki, blanketi 1, foronya1, chandarua 1(mashuka na chandarua vinapatikana katika duka la shule, shuka bei ni sh 9,000/=, chandarua @sh. 8,000/=. Au aje navyo.

**Mahitaji ya muhimu ya mwanafunzi**

i. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
ii. Mfuko au begi dogo la kubebea madaftari na vitabu.
iii. Vifaa vya kujifunzia darasani kama vile kalamu, madaftari, penseli, mathematical set, dictionary

**NB: Ni marufuku kubeba madaftari mkononi au kwa kutumia gazeti.**

**HGL**

- **Advanced learners dictionary (new edition)**

**HKL**

- Tahakiki ya Kiswahili kidato cha tano na cha sita.

**HGK**

- A Comprehensive Approach to physical Geography For Secondary School By B.T.

Msabila

**EGM**

- Advanced mathematics for secondary school form V & VI written by Petro L. Mayomya
- Chands -Volume I & II

**HGE**

- Essential For A-Level Economics by Ambrons Othiambo Paper 1 & 2
- Economics Made easy, by Edward Mwakagile

**GENERAL STUDIES**

- Understanding General Studies For Advanced Level

5th Edition

Author: Joannes Bigirwamungu & Sospeter M. Deogratias

Publisher; APE Network

Year published: 2020

**HISTORY**

- Essential in Advanced Level History paper 1&2 by Salehe Yassin
- Advanced learners History Form 5&6 by Oxford

## HESHIMA, KANUNI, NA SHERIA ZA SHULE

### A. HESHIMA.

Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Anatakiwa kusimama na kusalimia mwalimu, mfanyakazi na mtu yeyote anayemzidi umri.
ii. Anatakiwa kuheshimu wafanyakazi wote, wanafunzi wenzake na jamii yote anayoweza kukumbana nayo.
iii. Anapaswa kuthamini, kuheshimu na kutekeleza kazi zote anazopewa ndani na nje ya darasa.
iv. Anatakiwa kuvaa mavazi ya heshima wakati wote.
v. Kuheshimu ratiba nzima ya shule.
vi. Ni marufuku mwanafunzi kujipikilisha au kupeleka chakula bweni bila ruhusa ya mwalimu.

vii. Anatakiwa kutii amri au wito wa viongozi au walezi wake wakati wote awapo shuleni.
viii. Anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, Picha za viongozi, Nembo ya Taifa, Wimbo wa taifa na Fedha ya Taifa.
ix. Haruhusiwi kuingia katika nyumba za wafanyakazi/walimu, ofisi za walimu, maktaba na maabara n.k bila ruhusa.
x. Ni marufuku kupiga makelele mabwenini na madarasani wakati wote awapo shuleni.
xi. Anatakiwa kuheshimu na kukubali tofauti za kidini na kiutamaduni zilizopo katika jamii.
xii. Ni marufuku kushiriki au kuendekeza imani za kishirikina.
xiii. Ni marufuku mwanafunzi kutumia lugha chafu, kugombana mahali popote na kwa mtu yeyote.
xiv. Anatakiwa kuheshimu na kuitika wito toka kwa walezi/walimu pamoja na viongozi wake (viranja), hii ikiwa ni pamoja na mwitiko wa kengele wakati wote anapohitajika.
xv. Ni **marufuku mwanafunzi kumiliki simu hapa shuleni**. Akikamatwa na simu awapo shuleni, **atafukuzwa shule**.

**NB: Shule inatoa huduma ya mawasiliano yaliyo rasmi, ya lazima na yenye umuhimu tu.**

“Ni marukufu kwa mwanafunzi kuvuta sigara, kufuga kucha na kuzipaka rangi yoyote, kuwa na nywele ndefu (hawaruhusiwi kusuka wala kufunga rasta), kunyoa kipara, kuvaa wigi, kunyoa mtindo, (mf. Panki) na kamwe asiweke dawa wala piko kwenye nywele. Pia asipake rangi kwenye midomo, kope na asinyoe nyusi wala kutumia madawa ya kuchubua ngozi”.

**B. MAHUDHURIO**

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi popote anapotakiwa na kuhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani na nje ya darasa ikiwa ni pamoja na “morning parade”, “evening roll call” “afternoon prep, “evening prep”, “emergence calls”, n.k. kumezuka mtindo wa baadhi ya wanafunzi kwenda kusomea porini ambapo ni makao ya viumbe hatari kama nyoka. Ni marufuku kwenda kusomea porini.

ii. Kila mwanafunzi anatakiwa kutoa taarifa ya kutohudhuria shule au kipindi chochote ndani na nje ya darasa kwa mwalimu wa darasa/ mwl. Wa zamu na siyo kiongozi wa darasa yaani (monitress).
iii. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya mabweni na madarasa.
iv. Mwanafunzi akichelewa kutoka likizo ya muhula atalazimika kuleta mifuko miwili ya saruji( hata kama amechelewa siku moja).

**NB: Ni marufuku mwanafunzi kufika shuleni baada ya saa 12 jioni, hatapokelewa.**

**C. UVAAJI WA SARE**

i. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ya darasani muda wote awapo darasani, anapokwenda kanisani au msikitini, kwenda hospitali, na sare ya nje wakati wa shughuli mbalimbali za shule. Ni marufuku kuchanganya sare.

ii. Ni lazima mwanafunzi avae sare iliyo safi na nadhifu muda wote.

**ANGALIZO**

- Mwanao atavaa sare ya shule kwa kipindi chote atakapokuwa hapa shuleni na hataruhusiwa kuvaa nguo za nyumbani, **hivyo hairuhusiwi kuja na mzigo mkubwa wa nguo ambazo hatapata nafasi ya kuzivaa awapo shuleni.**
- Vipodozi, pafyum, radio, kamera, simu pamoja na nguo za nyumbani haviruhusiwi shuleni. Ukaguzi utafanyika kabla ya kuingia bwenini na pia unafanyika kwa kushitukiza. Akipatikana navyo, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.
- Hakikisha mwanao ajapo shuleni, awe amepimwa afya na kujaza fomu ya afya kikamilifu. Hii itatusaidia kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji maalumu kimalezi. Aidha, kutakuwa na upimaji afya wa dharura wanafunzi wawapo shuleni
- Kwa wale watakaoshonewa sare zao hapa shuleni **watatakiwa kuja na sketi za shule zao za awali kwa ajili ya kuvaa wakati wanasubiri kushonewa sare za shule.**

**ONYO.**

Mapambo ya aina zote kama pete, heleni, bangili, mikufu, viremba, n.k. haviruhusiwi kuvaliwa pamoja na sare ya shule. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia, nguo fupi zenye mipasuo, kupaka rangi kucha na midomo, nguo za kubana na viatu vyenye visigino virefu.

**NB: Wanafunzi watatakiwa kuja na sketi za shule aliyomalizia kwa ajili ya kuvaa wakati wanasubiri kushonewa sare.**

## D. MIPAKA YA SHULE

Mwanafunzi asitoke nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu kwa muda wote anaotakiwa kuwepo shuleni. Ni marufuku mwanafunzi kutembelea salon wakati wote wa vipindi.

Ni marufuku mwanafunzi kutembelea nyumba za kulala wageni (Guest houses), vilabu vya pombe (Bar) au majumba ya starehe (Recreation houses).

Mwanafunzi haruhusiwi kuingia ofisi ya walimu (Staff room) bila kibali maalumu.

## E. USAFI.

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi yeye mwenyewe na kutunza mazingira ya shule, hivyo anatakiwa kuleta Tsh 10,000/= kwa ajili ya vifaa vya usafi: ambavyo ni jembe na mpini wake, mfagio mmoja wa kuti (chelewa) pamoja na kimojawapo kati ya hivi (soft broom, hardbroom, squizer, moper).

## F. KUTEMBELEWA NA NDUGU (VISITING DAY)

Shule kwa sasa haina utaratibu wa wanafunzi wa bweni kutembelewa na ndugu na jamaa wakati wote wawapo shuleni. Pia kwa siku za jumapili, hakuna ruhusa ya kwenda kufanya manunuzi yeyote kwani mahitaji yote ya msingi yanapatikana katika duka la shule. Kwa mwanafunzi atakayekiuka haya na kukaribisha wageni nje ya utaratibu, ATAWAJIBISHWA. Daima mwanafunzi atumie muda wake vizuri kitaaluma awapo shule.

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xvi. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

## ZINGATIA

*Shule ina program na taratibu zake zenye kulenga kuinua na kuendeleza Taaluma shuleni. Mwanafunzi ni LAZIMA azifuate na kuzitekeleza. Hizi ni pamoja na kutumia lugha ya Kiingereza katika mawasiliano yote muda wote awapo shuleni. Kuhudhuria prep wakati wa mchana na hat usiku kwa nujibu wa ratiba. Pia kuhudhuria mihadhara mbalimbali ya masomo, yaani "DEBATES" na "SUBJECT CLUBS". Hii sio hiari ni LAZIMA*

4. **VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza

kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**** KAULI MBIU** ya shule ni "**lenga mbali**". Hii ni kwa kila Nyanja. Daima Lenga Mbali katika Elimu, Uchumi, Jamii na Utamaduni. Hii itaweza kufikiwa tu kwa kufuata masharti, sheria, taratibu na kanuni za shule. Nakutakia kila KHERI katika safari yako ya kitaaluma uwapo shuleni.

5. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

**KARIBUNI SANA!!!**

CLOTILDA E. KOMENKESHA
**MKUU WA SHULE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Shule ya sekondari Sumve,
S. L. P 44,
Mantare – Mwanza.

**FOMU YA KUKIRI KWA MZAZI/MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA, TARATIBU, KANUNI**

**NA MAELEKEZO MBALIMBALI YA SHULE JUU YA MWANAFUNZI.**

Mimi ……………………………………………… ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ………………………………………………… Nakiri kuwa nimezisoma mbele yake na kuzielewa vyema sheria, taratibu, kanuni na maelekezo mbalimbali atakayopewa mtoto wangu hapa shuleni.

Nimekubaliana nazo na endapo atafanya kinyume sitamtetea, badala yake nitakubaliana na kuheshimu maamuzi yatakayotolewa na uongozi wa shule au walezi wake.

Jina la mzazi/mlezi………………………………………………
Saini………………………………
Tarehe ……………………………

Jina la mwanafunzi……………………………………………….
Saini …………………………………………………………………
Tarehe …………………………………………………………….

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

**(FRMF) F1**

Please examine the student, (named)…………………………………………………. To her fitness to undergo training, studying and subsequently work.

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the following student named above and consider her fitness for re – engagement as above: this is certified by the following results of my examination:

1. Bilharzias ……………………………….
2. Jaundice……… …………………………
3. Scabies………………………………….
4. Typhoid………………………………….
5. Tropical ulcer…………………………….
6. Abscesses…………………………..
7. Asthma………………………………..
8. Leprosy………………………………….
9. Small pox………………………………..
10. Heart failure……………………………..
11. Cystitis…………………………………..
12. Diabetes…………………………………..
13. Epilepsy…………………………………..
14. STDs……………………………………..
15. Headache…………………………………..
16. Osteomyelitis……………………………..…
17. Bronchopneumonia……………………….
18. Skin disease……………………………….
19. TB………………………………………….

**OTHER EXAMINATIONS**

1.Eyes………………………….

2.Chest………………………….

3.Abdomen…………………….

4.Hemoglobin…………………..

5.Any abnormalities noted……….

………………………………..

6.Any chronic complaints not noted

……………………………….

**NOTE**:In case of TB and Bilharzias it is recommended that a student should attend a clinic/medical treatment before she come to school.

Name and signature of Medical officer / Examiner…………………………………

Designation and official Stamp …………………………………………,……..

Date ……………………………

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

FOMU YA URAIA

1. Jina la mwanafunzi……………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa ……………………… mwezi ……………………. Mwaka……….
3. Jina la Baba ………………………………………………………………………….
4. Mahali alipozaliwa:

   (a) Kijiji/ mtaa ………………………………..

   (b) Wilaya ……………………………………..

   (c) Mkoa ……………………………………
5. Ni raia wa Tanzania …………………………………………………………..……………….
6. Nambari na tarehe ya Hati ya Uraia iwapo si kwa kuzaliwa:
   ………………………………………………………………………………………………
7. Si raia wa Tanzania ni raia wa …………………………………………………………..…….
8. Jina la Mama ………………………………………………………………………………..
9. Mahali alipozaliwa:

   (a) Kijiji/ mtaa ………………………………..

   (b) Wilaya ……………………………………..

   (c) Mkoa ……………………………………

10. Ni raia wa Tanzania ……………………………………………………………………………….
11. Nambari na tarehe ya Hati ya Uraia iwapo si kwa kuzaliwa:

…………………………………………………………………………………………………………

12. Si raia wa Tanzania ni raia wa ……………………………………………………………………….

Saini ya Afisa mtendaji wa Kijiji/mtaa au saini ya Afisa mtendaji wa Kata
……………………………………….

Muhuri ………………………………………. Tarehe ………………………………….

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**SHULE YA SEKONDARI SUMVE**
**FOMU YA MAELEZO JUU YA MWANAFUNZI**

| **MATUMIZI YA OFISI TU** |
|---|
| NA. YA USAJILI |
| TAREHE YA KURIPOTI |

1. Jina kamili ………………………………………………… (ulilotumia katika shule uliyotoka).
2. Dini yako/Dhehebu……………………………………………………………………………….
3. Tarehe ya kuzaliwa ……..mwezi………mwaka…………..Wilaya……………Mkoa……………
4. Shule uliyotoka ……………………………………...Wilaya …………...Mkoa…………….
5. Michezo uipendayo au shughuli (hobbies) uzipendazo:

   …………………………………………………………………………………………………………
6. Ulemavu au historia ya ugonjwa (Tafadhali taja)……………………………………………
7. Unaishi na nani, mzazi au mlezi?........................ Taja jina lake,………………………………….

   Kama unaishi na mlezi, taja uhusiano: ………………………………………………………
8. Kazi ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………………….
9. Mahali anapoishi ……………………………………………………………………………….

   Wilaya …………………………………Mkoa………………………………

   Anwani ……………………………..Simu………………………………….
10. Jina na anwani ya mtu atakayetumiwa ripoti yako ya maendeleo ya masomo na mambo

mengine:

Jina lake kamili……………………………. Uhusiano……………………………..

Anwani ……………………………………. Simu ………………………………

11. Ndugu wanne (4) watakaokutembelea hapa shuleni na namba zao za simu:

| JINA | UHUSIANO | ANAPOISHI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

12. Jina la mji na kituo cha usafiri (uwanja wa ndege, bandari, stesheni ya reli na kituo cha basi) utakachoshukia wakati wa likizo zako ……………………………………………………..

**Tamko la mwanafunzi:**

“nimezisoma na kuzielewa Sheria na Kanuni za Shule, ninaahidi kuzifuata na kuzitekeleza”

Sahihi ya Mwanafunzi ………………………………    Tarehe ………………………………

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………………    Tarehe ………………………………

# SARE ZA SHULE



1. Wa kwanza kutoka kushoto ni mfano wa sare ya michezo ya uwanjani kwa wanafunzi wote.
2. Wa pili kutoka kushoto ni mfano wa sare za michezo kwa wanafunzi wote (ndani ya tracksuit)
3. Wa tatu kutoka kushoto ni mfano wa sare za kushindia kwa wanafunzi wa Waislam.
4. Wa nne kutoka kushoto ni mfano wa sare za kushindia kwa wanafunzi wa Kikristo.
5. Wa tano kutoka kushoto ni mfano wa sweta linalotakiwa kwa wanafunzi wote.
6. Wa sita kutoka kushoto ni mfano wa sare za darasani kwa wanafunzi wa Waislam.
7. Wa saba kutoka kushoto ni mfano wa sare za darasani kwa wanafunzi wa Kikristo.